

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI

27 MEI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA


KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI – TAREHE 27 MEI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



III. MASWALI:



OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

273. MHESHIMIWA DAUD PROTAS VENANT (IGALULA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Daraja katika Mto Loya.

**274. MHESHIMIWA REGINA NDEGE QWARAY
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaongeza kiwango cha mikopo ya Vikundi vya watu 5 inayotolewa na Halmashauri kutoka Shilingi milioni 1 hadi 5.

**275. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO
MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa soko la kisasa la Kwasadala.

**276. MHESHIMIWA MUSSA RAMADHANI SIMA
(SINGIDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-


Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na uhaba wa Walimu na Madarasa unaochagizwa na Sera ya Elimu bila malipo.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

277. MHESHIMIWA OMAR ISSA KOMBO (WINGWI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itakifanyia matengenezo Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Micheweni pamoja na ujenzi wa nyumba za Askari.



WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

278. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, ni kwa nini Serikali isitoe rasilimali za Kiwanda cha Mang'ula *Machine Tools* kilichopo Kilombero kwa Taasisi za Ufundi kama DIT.

WIZARA YA MAJI:

279. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali italishughulikia tatizo la maji kwa Vijiji zaidi ya 14 vya Tarafa ya Mtae.

280. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):

● Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- ●

Je, ni lini Serikali itakamilisha ahadi ya ujenzi wa Mradi wa Maji wa Vijiji 9 vya Kata za Oldonyosambu na Oldonyowas.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

281. MHESHIMIWA HASAN SELEMAN MTENGA (MTWARA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege Mtwara.

282. MHESHIMIWA NORA WAZIRI MZERU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Morogoro kupitia Malinyi hadi Namtumbo kwa kiwango cha lami.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
27 MEI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**